TANGAZO LA SERIKALI Na. 668 la tarehe. 2/8/204

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MJI GEITA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Geita ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Mji Geita.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote kinachouzwa sokoni, gulioni, mnadani, dukani au sehemu nyingine yoyote iliyoruhusiwa;

"chombo cha usafiri" maana yake ni gari la abiria au mizigo, bajaji, pikipiki; mkokoteni, baiskeli, punda au ng'ombe;

"mtambo wa kuchenjulia dhahabu (Carbon in Pulp)" maana yake ni mtambo wa kuchenjulia dhahabu ulioboreshwa zaidi ya skimu ya uchenjuaji unaotumika kuchenjulia dhahabu kutoka katika udongo wenye kudhaniwa kuwa na dhahabu ambao

huwekwa kwenye matenki kuchanganywa na maji, chokaa, na sumu sayanaidi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Geita;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kituo cha mabasi" Maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya abiria;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"minara" maana yake ni kifaa kinachopokea na kusafirisha mawasiliano ya simu au redio isipokuwa minara inayotumika kuongoza vyombo vya usafiri;

"mifugo" inajumuisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na aina yoyote ya wanyama ambao kwa kawaida hufugwa katika eneo la Halmashauri;

"masoko", "magulio" au "minada" maana yake ni maeneo maalumu yaliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"meza" au "kizimba" maana yake ni kitu au kifaa kinachotambulika kwa namba au alama kinachotumika kuwekea bidhaa za biashara katika soko au eneo lililoidhinishwa na Halmashauri;

"maegesho" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri;

"mazao mchanganyiko" maana yake ni mazao yote yanayotokana na shughuli za kilimo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Geita au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mwalo" maana yake ni muundo mbinu wa wachimbaji wadogo wa kukamatia dhahabu kwa kutumia madini ya zebaki ambao umejengwa kwa saruji,

kuzungushiwa mfereji wenye naironi na kuwekewa uzio madhubuti ili kuzuia uchafuzi wa mazingira;

"uchenjuaji" maana yake ni mfumo wa kutenganisha dhahabu kutoka katika mchanga, udongo au madini mengine;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa kupita katika maeneo ambayo huduma au biashara inafanyika kwa saa ishirini na nne.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au

kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Uzingatiaji wa masharti ya usafirishaji Sura ya 413

7. Kila mmiliki wa pikipiki atazingatia vigezo na masharti ya usafirishaji yaliyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini.

Masharti maalumu kwa usafirishaji

8.-(1) Kila mmiliki wa pikipiki au bajaji inayofanya biashara ya kusafirisha abiria atasajili chombo hicho kwa Halmashauri.

(2) Pikipiki iliyosajiliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itapangiwa eneo maalumu na Halmashauri la kuegeshwa wakati wa kufanya biashara.

(3) Kila mmiliki wa pikipiki inayofanya biashara ya kusafirisha abiria atawajibika kukata leseni ya kuendesha abiria.

Sura ya 168

(4) Mtu yeyote anayeendesha pikipiki ya kusafirishia abiria, pamoja na kuheshimu masharti mengine ya Sheria ya Usalama Barabarani, atawajibika pia kuhakikisha kwamba anavaa sare maalumu inayomtambulisha kama dereva wa pikipiki ya abiria.

(5) Ni marufuku kwa dereva kuegesha pikipiki au bajaji katika eneo ambalo hajapewa kibali na Halmashauri kuegesha.

Ushuru wa pikipiki na bajaji

9. Halmashauri itatoza ushuru kwa dereva wa pikipiki na bajaji zote zinazofanya biashara kila siku katika eneo la maegesho lililotegwa na Halmashauri.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

10.-(1) Mtu yoyote anayekusudia kuchimba madini ya ujenzi ndani ya Halmashauri atapaswa kuomba na kupata kibali cha kuchimba madini ya ujenzi kutoka Halmashauri kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

(2) Kibali kinachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitaeleza aina ya madini ya ujenzi yanayochimbwa na eneo

yatakapochimbwa.

Maeneo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi

11.-(1) Halmashauri itatenga na kutangaza maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi.

(2) Mchimbaji yeyote wa madini ya ujenzi atatakiwa kuzingatia sheria za hifadhi ya mazingira.

(3) Halmashauri itasimamisha shughuli za uchimbaji iwapo itathibitisha kuwa uchimbaji unaofanywa unasababisha uharibifu wa mazingira na uchimbaji unafanyika katika maeneo yafuatayo:

(a) maeneo ya hifadhi;
(b) maeneo ya mito au umbali wa mita 60 kando ya mito na vyanzo vya maji;
(c) maeneo yaliyo karibu na makazi ya watu;
(d) maeneo ya hifadhi ya barabara; na
(e) maeneo ambayo yametajwa katika sheria yeyote kuwa hayafai kwa shughuli ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Ushuru wa maegesho ya malori

12.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa ajili ya malori yote ya mizigo yanayofanya kazi katika eneo la Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa lori la mizigo atawajibika kulipa ushuru na kuruhusiwa kufanya kazi katika eneo la Halmashauri

Ushuru wa mazao mchanganyiko

13.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kutoza ushuru wa mazao mchanganyiko yatakayouzwa katika vyama vya ushirika vya msingi ambavyo vitateuliwa na kutangazwa na Mkurugenzi.

(2) Ushuru wa mazao mchanganyiko utatozwa kwa kiasi cha 3% ya bei ya kuuzuia, na utalipwa na mnunuzi kabla ya kusafirisha mazao na haki ya kudai na kupewa stakabadhi kwa malipo aliyofanya na stakabadhi.

(3) Mazao yatapaswa kusafirishwa katika gari la mizigo lililoidhinishwa na kutambuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(4) Mkulima anayesafirisha mazao anapaswa kuwa na barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji anacholimia na mazao hayo yatapaswa kusafirishwa

na mkulima mwenyewe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ndani au nje ya Halmashauri.

(5) Ni marufuku kwa mnunuzi kununua na kusafirisha mazao yaliyojazwa rumbesa au ujazo usioruhusiwa kwa mujibu wa Sheria za nchi.

Ukusanyaji wa madeni

14.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itashindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

15.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria

Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

16.-(1) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri baada ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) kupita katika maeneo ambayo huduma au biashara inafanyika kwa saa ishirini na nne.

Makosa

17. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

(e) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(f) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na

ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atatumia chombo chochote cha usafiri kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

18. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa kinyume na Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

19. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 371 la 2018

20. Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Mji Geita Mwaka 2018 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA
USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

| Na | Zao | Kiwango kwa Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Viazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | Karoti | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | Matunda | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | Vitunguu maji | 3% ya bei ya kununulia |
| 6 | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |
| 7 | Mchele | 3% ya bei ya kununulia |
| 8 | Mahindi/Alizeti/Mtama/Mpunga | 3% ya bei ya kununulia |
| 9 | Pamba | 3% ya bei ya kununulia |
| 10 | Zao jingine lolote litakalolimwa na kuuzwa katika mamlaka ya Halmashauri | 3% ya bei ya kununulia |
| 11 | Kibali cha kununua mazao | Tsh. 102,000/= kwa mwaka |
| 12 | Ushuru wa Samaki | 500/= kwa siku |
| 13 | Ushuru wa Pumba na Mashudu | 500/= kwa gunia |

SEHEMU YA PILI
USHURU WA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA USAFIRI AU ABIRIA (STENDI)

| Na | Chombo cha usafiri | Ushuru wa maegesho |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki iliyosajiliwa kwa biashara katika maeneo yaliyopangwa | 500/= kwa siku |
| 2 | Teksi | 1000/= kwa siku |
| 3 | Lori chini ya tani 7/pick up | 2,000/= kwa siku |
| 4 | Lori zaidi ya tani 7 basi kubwa | 5,000/= kwa siku |
| 5 | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/= kwa siku |
| 6 | Ushuru wa kituo cha mabasi au stendi | |
| | a) Mabasi makubwa ya abiria 20 hadi 30 | 3,000/= kwa safari |
| | b) Mabasi madogo | 2,000/= kwa safari |

*Tangazo la Serikali Na.668 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | c) | Teksi | 1,000/= kwa siku |
| | d) | Pikipiki | 500/= kwa siku |
| | e) | Bajaji | 1,000/= kwa siku |
| | f) | Gari nyingine | 500/= kwa siku |
| | g) | Mabasi makubwa ya abiria zaidi ya 30 | 4,000/= kwa siku |

SEHEMU YA TATU
ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI NA MICHEZO

| Na | Ada/Ushuru | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kibali cha ngoma za jadi | 50,000/= kwa siku |
| 2 | Kibali cha kuchezesha disko, maonesho ya bendi, sanaa na maonesho | 25,000/= kwa onesho |
| 3 | Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha | 30,000/= Kwa mwezi |
| 4 | Play station | 10,000/= kwa mwezi |
| 5 | Mechi za Halmashauri mpira katika uwanja wa mpira | 10% ya mapato ya kila mechi |
| 6 | Michezo ya pool table, fete | 10,000/= kwa mwezi |
| 7 | Kibali cha mechi za mpira | 10,000/= kwa mwezi |
| 8 | Uuzaji wa dawa za asili na tiba mbadala | 10,000/= kwa mwezi |
| 9 | Kibali cha kufanya huduma ya tiba mbadala | Shilingi 150,000/= kwa mwaka |
| 10 | Mashindano ya urembo | 100,000/= kwa tukio |
| 11 | Burudani za Taasisi / Kampuni | 50,000/= kwa tukio |
| 12 | Matangazo ya Promosheni | 50,000/= kwa siku kwa mkazi wa Halmashauri |
| | | 100,000/= kwa siku kwa asiye mkazi wa Halmashauri |
| 13 | Kusajili vikundi vya Sanaa | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 14 | Ada ya usajili kuwa mshehereshaji (MC) au mpiga muziki (DJ) | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 15 | Ada ya usajili wa studio ya kurekodi mziki usiokuna na filamu | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 16 | Ada ya usajili wa mawakala/wasambazaji wa kazi ya sanaa | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 17 | Ada ya maabara ya sanaa (Label) | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 18 | Ushuru wa upambaji kumbi za sherehe na mikutano | 20,000/= kwa siku/ Tukio |
| 19 | Kibali cha usajili wa ukumbi wa watu wasiozidi 350 | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 20 | Kibali cha usajili wa ukumbi wenye kukaa watu 351 hadi 550 | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 21 | Kibali cha usajili wa ukumbi wenye kukaa watu 551 hdi 750 | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 22 | Kibali cha usajili wa ukumbi wenye kukaa watu 751 na kuendelea | 25% ya gharama ya usajili wa kibali cha BASATA |
| 23 | Ushuru wa mshehereshaji (MC) au mpiga muziki (DJ), mpiga picha za video (Video Shooter) | 15,000/= kwa tukio |
| 24 | Matangazo ya vipaza sauti | 25,000/= kwa siku kwa mkazi wa halmashauri |
| | | 50,000/= kwa siku kwa asiye kuwa mkazi wa Halmashauri |

| | | |
|---|---|---|
| 25 | Kibali cha sherehe (harusi, kuzaliwa na pongezi) | 50,000/= kwa tukio |
| 26 | Ada za kumbi za starehe/burudani | 30,000/= kwa siku |
| 27 | Kibali cha kuonesha sinema, video, picha, jongefu, Mpira wa miguu | 10,000/= kwa siku |
| 28 | Kibali cha kuchukua/kupiga picha mnato na jongefu | 10,000/= kwa siku |
| 29 | Nyongeza ya tozo katika huduma na shughuli za Bodi ya Filamu | 25% ya fedha inayolipwa Bodi ya Filamu |
| 30 | Matangazo ya vipaza sauti eneo la stendi ya mabasi | Kwa mujibu wa mkataba |

SEHEMU YA NNE

ADA YA UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA UCHINJAJI/MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA MABUCHA.

| Na | Ada/Ushuru | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya ukaguzi wa nyama kwa kila ng'ombe atakayechinjwa | 1,500/= |
| 2 | Ushuru wa machinjio wa nyama kwa kila ng'ombe atakayechinjwa | 15,500/= |
| 3 | Ushuru wa ukaguzi wa nyama kwa kila kondoo, na mbuzi atakayechinjwa | 1,000/= |
| 4 | Ushuru wa machinjio kwa kila mbuzi/kondoo | 4,000/= |
| 5 | Ushuru wa machinji ya nyama kwa kila nguruwe | 3% ya mapato toka kwa mwenye chinjio |
| 6 | Ushuru wa ukaguzi wa nyama ya nguruwe | 800/= kila nguruwe |
| 7 | Ushuru wa bucha ya Ng'ombe, Mbuzi, Nguruwe na Kondoo | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA TANO

ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI.

| Na | Huduma | Kiwango cha Tsh. |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya vikao, mikutano na sherehe | 100,000/= hadi 1,000,000/= |
| 2. | Kukodi Gari: Magari ya kunyonyea maji machafu katika vyoo kwenye maeneo ya biashara<br>Magari ya kunyonya maji machafu katika vyoo kwenye makazi | Shilingi 100,000/= kwa kila safari moja<br>Shilingi 50,000/= kwa kila safari moja |
| 3. | Kukodi Mitambo ya Biashara | Shilingi 1,000,000/= kwa saa nane |
| 4. | Kukodi lori | Shilingi 300,000/=kwa siku |
| 5. | Kukodi viti vya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 6. | Kuweka kontena la biashara eneo la Halmashauri | Shilingi 300,000/= kwa mwaka kwa kila kontena |
| 7. | Kukodi vipaza sauti na matarumbeta | 100,000/= kwa siku |
| 8. | Kuweka kioski au magazeti | 10,000/= kwa mwezi |
| 9. | Kusoma nyaraka za wazi za Halmashauri | 1,000/= kwa siku moja |
| 10. | Kutumia maktaba ya Halmashauri | 1,000/= kwa siku moja |

SEHEMU YA SITA

ADA YA PANGO LA VIBANDA VYA BIASHARA.

| Na | Pango | Kiwango kwa Tshs. |
|---|---|---|
| 1 | Vibanda vinavyozunguka stendi au soko | Zitapangwa kutokana na Zabuni zitakavyoshindaniwa na kwa mujibu wa mkataba |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Ushuru wa meza au kizimba sokoni | 500/= kwa siku |

SEHEMU YA SABA

ADA YA KUPIMA AFYA ZA WAHUDUMU, WANAFUNZI NA WAFANYAKAZI

| Na | Huduma | Ada ya Huduma |
|---|---|---|
| 1 | Kusajiliwa na kupima afya kwa wahudumu wa kulala nyumba za wageni, vinyozi katika saluni za kike na kiume, hoteli, migahawa, wauzaji wa bucha, zahanati, mama na baba lishe, wauza matunda, baa, glosari, pombe za kienyeji, wafanyakazi katika sehemu za kuokea mikate na wahudumu katika mashine za nafaka | 5,000/ kwa kila muhudumu kwa miezi 6 |
| 2 | Kupima afya kwa wanaojiunga na vyuo, jeshi na shule za sekondari | 5,000/= |
| 3 | Kupima afya kwa wanaotaka kuajiriwa | 5,000/= |

SEHEMU YA NANE

USHURU WA MINADA YA MIFUGO NA MAZAO YA MIFUGO (Ulipwe na mnunuzi)

| Na | Ushuru wa Mifugo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 4,000/= kwa kila ng'ombe mnyama |
| 2 | Mbuzi/Kondoo | 1,000/= kwa kila Mnyama |
| 3 | Kuku/Kanga/Bata | 2,000/= kwa kila tenga la (Kuku/Kanga/Bata 5-20)<br>4,000/= kwa kila tenga la (Kuku/Kanga/Bata 21-30) |
| 4 | Nguruwe na Punda | 2,000/= kwa kila Nguruwe |
| 5 | Ushuru wa mikokoteni ya wanyama kazi | 20,000/= kwa mwaka |
| 6 | Ushuru wa ngozi za Ng'ombe/Mbuzi/Kondoo | 10,000/= kwa idadi ya ngozi kuanzia 100 hadi 1000 |
| 7 | Mama lishe au wauzaji wa vileo au nyama choma au vyombo vya nyumbani au wauza nguo za dukani au mitumba au viatu au wafanyabiashara wengine mnadani | 2,000/= kila siku |
| 8 | Vibali vya kusafirisha ngozi<br>a) Ng'ombe au Punda<br>b) Mbuzi au Kondoo au Nguruwe | <br>10,000/=<br>5,000/= |
| 9 | Kusafirisha pembe, nyeti za ng'ombe dume, mifupa na damu itokanayo na mifugo | 40,000/= kwa kibali |
| 10 | Muandaaji pembe, nyeti za ng'ombe dume, mifupa na damu itokanayo na mifugo | Alipe leseni ya biashara |
| 11 | Leseni ya mkokoteni wa wanyamakazi | 20,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA TISA

ADA YA KUOGESHA MIFUGO

| Na | Aina ya Mifugo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe/Punda | 150/= kwa kila mmoja |
| 2 | Mbuzi/ Kondoo | 100/= kwa kila mmoja |
| 3 | Mifugo ya kufuga sio kwa chakula | 100/= kwa kila mmoja |

SEHEMU YA KUMI

USHURU WA MADINI YA UJENZI.

| Na | Uzito wa gari | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mchanga $M^3$ 1 - 2.5 | 1,500/= kwa siku |
| 2 | Mchanga $M^3$ 2.6 – 4 | 5,000/= kwa kila safari |
| | Mchanga $M^3$ 10 | 10,000/= kwa kila safari |
| 3 | Kokoto $M^3$ 1 - 2.5 | 3,500/= kwa kila safari |
| 4 | Kokoto $M^3$ 2.6 na Zaidi | 10,000/= kwa kila safari |
| 5 | Mawe $M^3$ 1-2.5 | 3,000/= kwa siku |
| 6 | Mawe $M^3$ 2.6 hadi $M^3$ 10 | 8,000/= kwa kila safari |
| 7 | Matofali $M^3$ 1-2.5 | 5,000/= kwa kila safari |
| 8 | Kibali cha eneo la kuchimba madini ujenzi | 100,000/= kwa mwaka |
| 9 | Kila $M^3$ inayoongezeka kutoka $M^3$ 10 katika madini ya ujenzi | 1,000/= kwa safari |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

USHURU WA MCHANGA WENYE MADINI

| Na | Uzito wa gari | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | $M^3$ 1-2.5 | 2,500/= kwa kila safari |
| 2 | $M^3$ 4 | 5,000/= kwa kila safari |
| 3 | $M^3$ 5-7 | 10,000/= kwa kila safari |
| 4 | $M^3$ 8 –na kuendelea | 15,000/= kwa kila safari |
| 5 | Ushuru wa mfuko wa mchanga/mawe wa madini (kiroba) kutoka katika eneo la uchimbaji/eneo la leseni lililopo ndani ya Halmashauri | 2,000/= kwa kila kiroba |
| 6 | Kila $M^3$moja ya mchanga wa madini itakayosafirishwa nje ya eneo la Halmashauri italupiwa ushuru | 2,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA.

| Na | Aina ya gari | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Gari la mizigo lisilozidi $M^3$ 3 | 1,000/= kwa siku ya gulio au soko |
| 2 | Gari la mizigo linalozidi $M^3$ 3 | 2,000/= kwa siku ya gulio au soko |
| 3 | Magari mengineyo | 500/= kwa kila moja |
| 4 | Kibali cha kununulia vyuma chakavu/plastiki | 10,000/= kwa mwezi |
| 5 | Kibali cha kusafirisha vyuma chakavu/plastiki kuanzia $M^3$ 1 | 10,000/= kwa safari |

SEHEMU YA KUMI NA TATU

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

*Tangazo la Serikali Na.668 (Linaendelea.)*

| NA | UKUBWA WA JENGO (mita za mraba | ENEO LA KATI LA MJI (CBD) | | | ENEO KARIBU NA CBD (NEXT TO CBD) | | | PEMBEZONI MWA MJI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | UJAZO WA JUU | UJAZO WA KATI | UJAZO WA NCHINI | UJAZO WA JUU | UJAZO WA KATI | UJAZO WA NCHINI | UJAZO WA JUU | UJAZO WA KATI | UJAZO WA NCHINI |
| 1 | 1-25 sqm | 30,000 | 35,000 | 40,000 | 20,000 | 25,000 | 30,000 | 10,000 | 15,000 | 20,000 |
| 2 | 26-50 sqm | 40,000 | 45,000 | 50,000 | 30,000 | 35,000 | 40,000 | 20,000 | 25,000 | 30,000 |
| 3 | 51 - 75 sqm | 50,000 | 55,000 | 60,000 | 40,000 | 45,000 | 50,000 | 30,000 | 35,000 | 40,000 |
| 4 | 76 - 100 sqm | 60,000 | 65,000 | 70,000 | 50,000 | 55,000 | 60,000 | 40,000 | 45,000 | 50,000 |
| 5 | 101 - 125 sqm | 70,000 | 75,000 | 80,000 | 60,000 | 65,000 | 70,000 | 50,000 | 55,000 | 60,000 |
| 6 | 126 - 150 sqm | 80,000 | 85,000 | 90,000 | 70,000 | 75,000 | 80,000 | 60,000 | 65,000 | 70,000 |
| 7 | 151 - 175 sqm | 90,000 | 95,000 | 100,000 | 80,000 | 85,000 | 90,000 | 70,000 | 75,000 | 80,000 |
| 8 | 176 - 200 sqm | 100,000 | 105,000 | 110,000 | 90,000 | 95,000 | 100,000 | 80,000 | 85,000 | 90,000 |
| 9 | 201 - 225 sqm | 110,000 | 115,000 | 120,000 | 100,000 | 105,000 | 110,000 | 90,000 | 95,000 | 100,000 |
| 10 | 226 - 250 sqm | 120,000 | 130,000 | 150,000 | 110,000 | 115,000 | 120,000 | 100,000 | 105,000 | 110,000 |
| 11 | 251 - 275 sqm | 150,000 | 175,000 | 200,000 | 120,000 | 125,000 | 150,000 | 110,000 | 115,000 | 120,000 |
| 12 | 276 - 300 sqm | 200,000 | 220,000 | 250,000 | 150,000 | 160,000 | 175,000 | 120,000 | 130,000 | 150,000 |
| 13 | Zaidi ya 300 sqm | 250,000 | 300,000 | 350,000 | 200,000 | 250,000 | 300,000 | 150,000 | 200,000 | 250,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Kituo cha mafuta | 300,000/= |
| 15. | Majengo maalum kana shule/zahanati | 200,000 |
| 16. | Kibali cha kuzungusia mabati wakati wa kujenga | 500/= mita |
| 17. | Ada ya maombi ya viwanja | 20,000/= kwa fomu |
| 18. | Kibali cha ujenzi wa uzio | 1,000/= kwa mita |
| 19. | Kibali cha ukarabati majenzi (renovation) | 100,000-500,000/= |
| 20. | Maombi ya mabadiliko ya matumizi kutoka makazi kuwa makazi ya biashara | 100,000/= |
| 21. | Maombi ya mabadiliko ya matumizi kutoka makazi kuwa viwanda vya huduma (service trade industry) | 150,000/= |
| 22. | Maombi ya mabadiliko ya matumizi kutoka biashara kwenda makazi | 150,000/= |
| 23. | Maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutokabiashara/makazi kwenda matumizi mengine | 200,000/= |
| 24. | Ada ya urasimishaji makazi holela | Kwa kufuata miongozo ya Wizara ya Ardhi |
| 25. | Ada ya ukaguzi wa viwanja vya ujazo wajuu, kati na chini vya makazi na biashara vilivyopimwa na kampuni au mpima binafsi | 30,000/= kwakila kiwanja |
| 26. | Ada ya ukaguzi wa viwanja vya taasisi na viwanda vilivyopimwa na kampuni au mpima binafsi | 100,000/= kwakila kiwanja |
| 27. | Ada ya kurudisha mipaka (beacons) | 175,000-250,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NNE

KODI, ADA YA VIBALI VYA UJENZI WA JENGO LILILOPO UPIMAJI NA USAFISHAJI WA VIWANJA, MINARA, REDIO NA RNNINGA

| Na. | Aina ya Jengo | Kwa kila kibali |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba ya kuishi | 25,000/= |
| 2 | Nyumba ya biashara | 50,000/= |
| 3 | Ghorofa 1 | 200,000/= |
| 4 | Kiwanda, bohari, ghala | 200,000/= |
| 5 | Ada ya kukaguwa kiwanja kidogo (High Density) | 10,000/= |
| 6 | Nyumba biashara na kuishi | 70,000/= |
| 7 | Ada ya kukagua kiwanja cha kati (Medium density) | 20,000/= |
| 8 | Ada ya kukagua kiwanja kikubwa (Low density) | 50,000/= |
| 9 | Ada ya kukagua kiwanja kikubwa zaidi (super low density) | 70,000/= |
| 10 | Kibali cha kuzungusha mabati wakati wa kujenga | 500 kwa mita moja |
| 11 | Ada ya maombi ya viwanja | 20,000/= kwa fomu |
| 12 | Kibali cha kusimika mnara wasimu | 2,000,000/= kwa mwaka |

*Tangazo la Serikali Na.668 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 13 | Ada ya mnara wa simu wenye booster | 2,500,000/= kwa mwaka |
| 14 | Ada ya mnara wa simu usio na booster | 2,000,000/= kwa mwaka |
| 15 | Kibali cha ujenzi wa ukumni wa sinema mpira/starehe | 150,000/= |
| 16 | Kibali cha ujenzi wa Taasisi mbalimbali kama shule, vyuo na Ofisi ambazo sio ghorofa | 150,000/= |
| 17 | Kibali cha ujenzi wa kiwanda kikubwa | 500,000/= |
| 18 | Kibali cha ujenzi wa kiwanda cha kati/kidogo | 100,000/= |
| 19 | Kibali cha ujenzi wa sikimu ya uchenjuaji (CIP, Illussion, Vat each plant) | 100,000/= |
| 20 | Kibali cha ujenzi wa ghala/bohari | 100,000/= |
| 21 | Kibali cha ujenzi wa majengo ambayo hayajatajwa pamoja na marekebisho ya ujenzi | Inategemea na aina ya jengo |
| 22 | Nukuu ya bei kwa kila fomu | 5,000/= |
| 23 | Ada ya kiwanda cha uchenjuaji wa dhahabu (Vat leaching Plant) | 3,000,000/=kwa mwaka |
| 24 | Ada ya kiwanda cha uchenjuaji dhahabu (Vat leaching plant) chenye tanki zaidi ya 15 | 3,600,000/= kwa mwaka |
| 25 | Ada ya kiwanda cha ujenjuaji (Carbon in pulp, illusion) | 5,000,000/= |
| 26 | Kibali cha ujenzi wa mwalo | 100,000/= |
| 27 | Kibali cha kusimika karasha | 100,000/= |
| 28 | Ushuru wa ghara la kuhifadhia nafaka | 50,000/= kwa mwaka |
| 29 | Ada ya ukaguzi wa mazingira wa ujenzi wa sikimu ya uchenjuaji (illusion na CIP) | 300,000/= |
| 30 | Ada ya kufanya ukaguzi wa mazingira ya eneo la ujenzi wa mialo na makarasha | 50,000/= |
| 31 | Kila ghorofa inayoongezeka kutoka ghorofa ya 1 | 100,000/= |
| 32 | Kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ya makazi kwenda biashara | 300,000/= |
| 33 | Kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ya makazi kwenda viwanda | 400,000/= |
| 34 | Kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ya biashara kwenda makazi | 300,000/= |
| 35 | Kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ya makazi/biashara/viwanda kwenda matumizi mengine | 300,000/= |
| 36 | Kodi ya viwanda vingine tofauti na viwanda vya uchenjuaji madini | 1,000,000/= kwa mwaka |
| 37 | Ada ya urasimishaji | 100,000 kwa kila kiwanja isizidi 150,000/= |
| 38 | Ada ya kuzingira/majukwaa kwa muda usiozidi mwaka mmoja | 5,000/= kwa kila futi za mraba |

SEHEMU YA KUMI NA TANO
USHURU WA MAZAO YA MISITU YA HALMASHAURI.

| Na. | Aina ya zao | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa gunia la mkaa lenye uzito usiozidi kg 50 | 3% ya bei kwa kila gunia |
| 2 | Ushuru wa nguzo za miti kwa kila nguzo | 1,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Ushuru wa lita 1 ya asali | 400/= |
| 4 | Ushuru waNta Kg 1 | 500/= |
| 5 | Ushuru wa gogo | 2,000/= |
| 6 | Fito $M^3$ 1-10 | 2,000/= |
| 7 | Fito $M^3$ 11 | 5,000/= |
| 8 | Ushuru wa mbao 1 | 500/= ubao laini 1,500/= ubao mgumu |
| 9 | Ushuru wa banzi | 200/= |
| 10 | Ushuruwa kuni kwa kila ujazo wa mita moja | 1,500/= |
| 11 | Ada ya usajili wa biashara ya mazao ya misiti | 5% ya ada inayolipwa Serikali Kuu |

SEHEMU YA KUMI NA SITA
USHURU WA MAKARASHA YA MARUDIO.

| Na. | Huduma | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa makarasha | 20,000/= kwa mwezi |
| 2 | Ushuru wa mialo | 20,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA KUMI NA SABA
ADA YA USAJILI WA VIKUNDI.

| Na. | Aina ya kikundi | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Usajili wa vyama, vikundi au asasi za kiraia (CSOs/CBOs) | 20,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NANE
USHURU WA MABANGO

| NA. | MAELEZO | ADA (KWA TSHS.) |
|---|---|---|
| 1 | Mabango yasiyo na mwanga | 15,000/= kwa futi ya mraba |
| 2 | Mabango yenye mwanga | 18,000/= kwa futi ya mraba |
| 3 | Mabango yenye kuta | 15,000/= kwa futi mraba |
| 4 | Mabango ya kielekroniki | 20,000/= kwa futi ya mraba |
| 5 | Magari ya matangazo | 15,000/= kwa futi ya mraba |
| 6 | Matangazo kwenye Kituo cha mauzo<br>I. Mabango yasiyo na mwanga<br>II. Mabango yenye mwanga | <br>15,000/= kwa futi ya mraba<br>18,000/= kwa futi ya mraba |
| 7 | Kila tangazo la biashara kwa matangazo ya awali 100 | 100,000/= |
| 8 | Matangazo ya biashara au Promosheni kwa siku<br>Kwa kila tangazo jingine lenye matangazo ya jumla 100 au sehemu | 55,000/=<br><br>55,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Matangazo ya mabango yanayoelekeza sehemu za huduma kijamii zinazopatikana katika Shule, Zahanati, Hospitali | Hakuna Ada |
| 10 | Magari yaliyobandikwa matangazo ya bidhaa wanazozalisha | 4,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TISA
ADA ZA UTUPAJI TAKA NGUMU KWENYE JAA LA TAKA, UBOMOAJI NA UONDOAJI WA MABAKI YA VIFAA VYA UJENZI NA UKUSANYAJI TAKA KATIKA KAYA, MAJENGO YA BIASHARA NA TAASISI ZA WATU BINAFSI

Ada za utupaji taka ngumu kwenye jaa la taka

| Na | Kiasi cha Taka | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya tani moja kwa safari | 40,000/= |
| 2 | Zaidi ya tani moja kwa safari | 50,000/= |

Ubomoaji na uondoaji wa mabaki ya vifaa vya ujenzi

| Na | Eneo kwa mita ya Ujazo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mita moja ya mraba | 5,000/= |

Ukusanyaji taka katika kaya, Majengo ya biashara na Taasisi za watu binafsi.

| Na | Aina ya Biashara | Viwango vya ada |
|---|---|---|
| 1 | Makazi (kaya) | 2,000/= kwa mwezi |
| 2 | Mgahawa mdogo | 3,000/= kwa mwezi |
| 3 | Mgahawa wa kati | 5,000/= kwa mwezi |
| 4 | Mgahawa mkubwa | 15,000/= kwa mwezi |
| 5 | Nyumba ya kulala wageni yenye vyumba vya bei ya chini ya shilingi 10,000/= | 10,000/= kwa mwezi |
| 6 | Nyumba ya kulala wageni yenye vyumba vya bei ya kuanzia shilingi 10,000/= hadi 20,000/= | 15,000/= kwa mwezi |
| 7 | Nyumba ya kulala wageni yenye vyumba vya bei ya kuanzia shilingi 20,000/= hadi 50,000/= | 20,000/= kwa mwezi |
| 8 | Nyumba ya kulala wageni yenye vyumba vya bei ya kuanzia shilingi 50,000/= hadi 100,000/= | 50,000/= kwa mwezi |
| 9 | Nyumba ya kulala wageni yenye vyumba vya bei ya kuanzia shilingi 100,000/= hadi 200,000/= | 100,000/= kwa mwezi |
| 10 | Kiwanda kikubwa | 200,000/= kwa mwezi |
| 11 | Kiwanda cha kati | 100,000/= kwa mwezi |
| 12 | Kiwanda kidogo | 20,000/= kwa mwezi |
| 13 | Zahanati binafsi (Taka zisizo hatarishi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 14 | Kituo cha Afya binafsi (Taka zisizo hatarishi) | 15,000/= kwa mwezi |
| 15 | Hospitali binafsi | 25,000/= kwa mwezi |
| 16 | Hospitali ya rufaa | 30,000/= kwa mwezi |
| 17 | Wauza mbao | 5,000/= kwa mwezi |
| 18 | Wapasua mbao | 10,000/= kwa mwezi |
| 19 | Fundi seremala wakubwa | 25,000/= kwa mwezi |
| 20 | Fundi seremala wa kati | 10,000/= kwa mwezi |
| 21 | Fundi seremala wadogo | 5,000/= kwa mwezi |
| 22 | Fundi chuma | 5,000/= kwa mwezi |
| 23 | Karakana kubwa | 50,000/= kwa mwezi |

*Tangazo la Serikali Na.668 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 24 | Karakana ya kati | 20,000/= kwa mwezi |
| 25 | Karakana ndogo | 10,000/= kwa mwezi |
| 26 | Duka la jumla | 20,000/= kwa mwezi |
| 27 | Duka kubwa (Super Market) | 30,000/= kwa mwezi |
| 28 | Duka la kati (Rejareja) | 10,000/= kwa mwezi |
| 29 | Duka dogo (rejereja) | 5,000/= kwa mwezi |
| 30 | Shule ya Msingi ya Bweni (Binafsi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 31 | Shule ya msingi ya Kutwa (binafsi) | 5,000/= kwa mwezi |
| 32 | Shule ya Sekondari kutwa (Binafsi) | 10,000/= kwa mwezi |
| 33 | Shule ya Sekondari Bweni (Binafsi) | 20,000/= kwa mwezi |
| 34 | Duka dogo la chakula | 5,000/= kwa mwezi |
| 35 | Duka la kati la chakula | 10,000/= kwa mwezi |
| 36 | Duka kubwa la chakula | 20,000/= kwa mwezi |
| 37 | Baa kubwa | 50,000/= kwa mwezi |
| 38 | Baa ya kati | 20,000/= kwa mwezi |
| 39 | Baa ndogo (Grocery) | 10,000/= kwa mwezi |
| 40 | Klabu ya siku | 50,000/= kwa mwezi |
| 41 | Kumbi za Sherehe | 50,000/= kwa mwezi |
| 42 | Duka la kuuza nyama na samaki | 10,000/= kwa mwezi |
| 43 | Duka la dawa (Jumla) | 20,000/= kwa mwezi |
| 44 | Duka la dawa (Rejareja) | 10,000/= kwa mwezi |
| 45 | Dobi mdogo | 1,000/= kwa mwezi |
| 46 | Fundi wa vifaa vya umeme | 5,000/= kwa mwezi |
| 47 | Fundi kushona kwa kila cherehani | 1,000/= kwa mwezi |
| 48 | Saluni | 5,000/= kwa mwezi |
| 49 | Kituo cha kuuza mafuta kikubwa (Petrol Station) | 50,000/= kwa mwezi |
| 50 | Kituo cha kuuza mafuta cha kati (Filling Station) | 20,000/= kwa mwezi |
| 51 | Stoo | 5,000/= kwa mwezi |
| 52 | Ghala | 25,000/= kwa mwezi |
| 53 | Taasisi za kidini | 10,000/= kwa mwezi |
| 54 | Taasisi zisizo za kidini | 50,000/= kwa mwezi |
| 55 | Klabu ya pombe ya asili | 2,000/= kwa mwezi |
| 56 | Kituo cha michezo | 20,000/= kwa mwezi |
| 57 | Uwanja wa michezo | 10,000/= kwa mwezi |
| 58 | Washona viatu | 1,000/= kwa mwezi |
| 59 | Stoo za mkaa | 10,000/= kwa mwezi |
| 60 | Duka la kuuza magari | 50,000/= kwa mwezi |
| 61 | Nyumba za video/Sinema | 5,000/= kwa mwezi |
| 62 | Gereji kubwa ya magari | 50,000/= kwa mwezi |
| 63 | Gereji ya kati ya magari | 20,000/= kwa mwezi |
| 64 | Gereji ndogo ya magari | 10,000/= kwa mwezi |
| 65 | Gereji ya pikipiki | 10,000/= kwa mwezi |
| 66 | Gereji ya baiskeli | 5,000/= kwa mwezi |
| 67 | Sehemu kubwa za kuoshea magari | 10,000/= kwa mwezi |
| 68 | Sehemu ndogo za kuoshea magari | 5,000/= kwa mwezi |
| 69 | Mashine za kusaga ndogo | 5,000/= kwa mwezi |
| 70 | Mashine za kusaga kubwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 71 | Viwanda vya simu | 3,000/= kwa mwezi |
| 72 | Wauza barafu | 5,000/= kwa mwezi |
| 73 | Wauza mkaa wa jumla | 10,000/= kwa mwezi |
| 74 | Wauza mkaa wa rejareja | 5,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 75 | Vizimba sokoni | 200 kwa siku |
| 76 | Wauza Ngozi | 5,000/= kwa siku |
| 77 | Ofisi | 5,000/= kwa mwezi |
| 78 | Dahalia | 20,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA ISHIRINI

ADA NA USHURU WA HUDUMU NYINGINE

| Na | | |
|---|---|---|
| 1 | Adhabu ya papo kwa papo kw mifugo inayokamatwa kwa kuzurura ovyo;<br>a) Ngombe au punda<br>b) Nguruwe<br>c) Mbuzi na Kondoo | <br><br>5,000/= kwa kila mmoja<br>3,000/= kwa kila mmoja<br>2,000/= kwa kila mmoja |
| 2 | Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo:<br>d) Ngombe au punda<br>e) Nguruwe<br>a) Mbuzi na Kondoo | <br><br>3,000/= kwa kila mmoja kwa siku<br>2,000/= kwa kila mmoja kwa siku<br>1,000/= kwa kila mmoja kwa siku |
| 3 | Ushuru wa huduma ya maghala na vinu vya kusaga na kukoboa mpunga na mahindi | 25,000/= kwa mwaka |
| 4 | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 10% kwa kila kitanda |
| 5 | Ada za utambuzi wa mifugo na uwekaji kitanda | Kulingana na mwongozo wa wizara |
| 6 | Ada ya kibali cha mlipuko wa mawe | 50,000/= kwa kibali |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA

ADA NA USHURU WA KUPAKIA NA KUSHUSHA BIDHAA MBALIMBALI

| Na | Aina ya bidhaa | Gari ujazo (Ukubwa wa Tani) | Gharama za Ushuru (Shilingi za Tanzania) |
|---|---|---|---|
| 1 | Bidhaa ya ujenzi | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 8,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 10,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 12,000/= |
| 2 | Bidhaa ya chakula | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 10,000/= |
| 3 | Bidhaa za Vinywaji (Beverages) | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 10,000/= |
| 4 | Bidhaa za matumizi ya nyumbani | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 10,000/= |
| 5 | Vifaa vinavyotumia umeme | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 10,000/= |

*Tangazo la Serikali Na.668 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Bidhaa za mafuta ya magari, mitambo na gesi | Tani 1 hadi Tani 6.9 | 10,000/= |
| | | Tani 7 hadi Tani 15 | 20,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi | 25,000/= |
| 7 | Vyuma chakavu | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 16 na zaidi | 20,000/= |
| 8 | Mazao mchanganyiko ya kilimo | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 16 na zaidi | 10,000/= |
| 9 | Mazao ya Maliasili | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 3,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 5,000/= |
| | | Tani 11 hadi Tani 15.9 | 8,000/= |
| | | Tani 16 na zaidi | 10,000/= |
| 10 | Bidhaa, mazao ya kilimo na maliasili | Gunia | 500/= |
| | | Tenga | 500/= |
| | | Dumu/Ndoo ya Lita 20 | 500/= |
| | | Box | 500/= |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI

ADA YA USHURU WA MEZA KATIKA MASOKO YETU

| Na | Ushuru | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa Meza | 300 |
| 2 | Tozo ya Usafi | 200 |
| | Jumla | 500 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(1)*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

1. Jina la mwombaji……………………………………………………………

2. Anwani ya mwombaji……………………………………………………..
   Simu…………………………………….. barua pepe………………………………..

3. Aina ya madini yanayoombewa kibali………………………………………

4. Eneo linaloombewa kibali:
   i. Mahali/Kitongoji………………………kijiji/mtaa……………………kata……
   …..........................
   ii. Ukubwa wa eneo …………………………………………………...
   iii. Nambari ya leseni ya mchimbaji mwombaji ………………………….

5. Muda wa kibali:
   Tarehe ya kutolewa kwa kibali…………………………
   Mwanzo wa kibali………………………………………
   Mwisho wa kibali…………………………………….

6. Masharti ya jumla ya kibali:
   i. Mwombaji awasilishe mpango wa usimamizi wa mazingira katika eneo analotaka kuchimba
   ii. Mwombaji awasilishe mpango wa uchimbaji wa madini husika
   iii. Kazi ya kuchimba itafanyika kati ya saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni
   iv. Mwombaji atalazimika kuhakikisha ushuru wa Halmashauri unalipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Halmashauri

7. Masharti mahususi kwa mwombaji:
   i. ……………………………………………………………………….
   ii. ……………………………………………………………………….
   iii. ……………………………………………………………………….
   iv. ……………………………………………………………………….

Jina la anayetoa kibali ………………………………………………………..
Sahihi………………… Wadhifa wa mtoa kibali…………Tarehe ……………….

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi .....................................................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Geita kwamba arehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Geita ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Geita, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka …….............
Jina: ...........................................................
Saini: .........................................................

MBELE YA:
Jina……......................................................
Wadhifa: .................................................. .
Saini: .........................................................
Tarehe: .......................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Geita uliofanyika tarehe 29/8/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

YEFRED EDSON MYENZI,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya mji,*
*Geita*

MHE. COSTANTINE MORANDI MTANI,
*Mwenyekiti*,
*Halmashauri ya mji,*
*Geita*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
20 Juni, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*